United Nations

A Time for Renewal

UNITED NATIONS INFORMATION CENTRE – DAR ES SALAAM

P.O. Box 9224
Old Boma Building
Sokoine/Morogoro Road
Dar es Salaam

Tel: 255-22-2119510/2112923
Fax: 255-22-2112923
E-mail: unic.urt@raha.com
Website: www.unic.undp.org

UJUMBE WA SIKU YA AMANI DUNIANI

Katibu Mkuu Kofi Annan

21 September 2005

Amani ndilo suala la msingi wa Umoja wa Mataifa.

Ndio msingi wa uhai wetu. Ndio inatutambulisha ubinadamu wetu. Kiini cha jinsi tulivyo katika kila tendo tunalofanya.

Tarehe 21 Septemba, Siku ya Amani Duniani, ni wakati ambapo tunastahili kukiri upya dhamira yetu kuhusu suala hili.

Ni fursa ya kuangalia jinsi ya kuimarisha mipango ya pamoja ya usalama wetu.

Na inatakiwa iwe ni siku ya kuacha mapigano popote pale duniani. Natoa wito kwa mataifa yote na watu wote kuachana na migogoro ya chuki kwa siku nzima ya leo. Aidha nawasihi watu wote duniani kote kusimama kimya na kutafakari kwa muda wa dakika moja ifikapo saa 6 mchana.

Saa 24 sio muda mrefu.

Lakini ni muda wa kutosha kwa wapiganaji vitani na viongozi wa kisiasa kutafakari madhara yanayowapata watu wao na nchi zao.

Ni muda mrefu wa kutosha wa kutazama mbele ya ngome za kivita na seng'enge kati ya upande mmoja na mwingine na kuona iwapo kuna njia mbadala ya maelewano.

Katika kuadhimisha leo Siku ya Amani Duniani, tunapaswa sisi sote tuwakumbuke wale ambao wameteseka na mapigano. Hebu natujenge dhamira ya amani katika mioyo yetu.

Ahsanteni